# Ndaki ataka mchango zaidi sekta ya mifugo

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema bado mchango wa sekta ya mifugo kwenye pato la taifa ni mdogo ukilinganisha na idadi ya mifugo iliyopo nchini.

Aidha, ameitaka Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Nyama Tanzania kusimamia soko la nyama ndani na nje ya nchi ili mauzo yaongezeke.

"Tanzania ina mifugo milioni 67 na hii ni ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku tu na hapo bado hatujahesabu mifugo mingine kama kanga," alisema.

Alisema hayo jana jijini hapa wakati wa uzinduzi wa bodi hiyo.

Alisema hapa nchini kuna idadi kubwa ya mifugo lakini sekta ya mifugo imekuwa ikichangia asilimia 7.1 kwenye pato la taifa.

"Hicho ni kiwango kidogo ukilinganisha na kiwango cha mifugo tuliyonayo lakini mchango ni mdogo lazima tufanye mabadiliko."

Aliwataka kwenda kusimamia soko la nyama ndani na nje ya nchi na kuwezesha ukuaji wa soko la nyama.

"Tukipata wawekezaji wanaopeleka mazao yanayochakatwa nje ya nchi tutaongeza ajira, ni muhimu kutengeneza mazingira mazuri yatakayovutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi," alisema.

Alisema azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha taasisi na mashirika yaliyo chini ya serikali yanaimarishwa ili kuweza kuchangia uzalishaji wa mali na kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema wanatambua umuhimu wa taasisi za serikali na mashirika ya umma katika kuchangia mapato ya serikali na hivyo kuiongezea serikali uwezo wa kuwahudumia wananchi.

Alisema serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa taasisi na mashirika yake hayalegilegi kiutendaji kwa sababu yoyote ile, hivyo serikali itatekeleza wajibu huo, litawezesha mashirika na taasisi zake kwa njia mbalimbali kulingana na mahitaji kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Alisema wizara imejipanga kusimamia na kufuatilia kwa umakini utendaji wa taasisi zote zilizo chini ya sekta ya mifugo ili kuhakikisha zinajiendesha vizuri, si kwa hasara bali kwa faida ili serikali ifaidike na mapato na mchango wa taasisi hizo.

Alisema bodi hiyo inategemewa sana katika kusimamia na kukuza soko la nyama ndani na nje ya nchi.

"Utendaji kazi wenu ukaongozwe na sheria, kanuni na taratibu, kuzingatia sheria ya tasnia ya nyama namba 10 ya mwaka 2006, kanuni zake sita pamoja na sheria nyingine za nchi, kwa kufanya hivyo mtaweza kutekeleza kazi zenu kwa weledi na ufanisi mkubwa," alisema.

Alitaka bodi hiyo kuandaa mpango wa mabadiliko wa bodi, kusimamia mipango, mikakati mizuri ya kuongeza huduma za biashara ya nyama hapa nchini kwa kutumia vizuri fursa zilizoibuka, kusimamia na kutatua migogoro mahali pa kazi.

Scanned with CamScanner

na kwa kuwa wanaaminiwa na | kuwaanidi waganga hao kulifikisha | na kwamba suala hilo lazima lifike | hiyo wanakuwa hawafanyi sawa bali wanawaharibia wenzao.

# Ulega azindua uvalishaji hereni za kielektroniki

**Arusha**
**NA LILIAN JOEL**

NAIBU wa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, amezindua zoezi la uvalishaji mifugo hereni za kielektroniki wilayani Ngorongoro mkoani hapa ambazo zitasaidia kuonyesha umiliki na sehemu inapotoka.

Pia, amezindua zoezi la uhimilishaji wa mifugo katika wilaya hiyo kwa lengo la kuwasaidia wafungaji kuwa mifugo michache bora yenye tija badala ya mifugo mingi isiyo na tija ambayo inakuwa vigumu kwa wafugaji kuitunza wakati wa ukame na kusababisha vifo.

Ulega akizindua miradi hiyo katika Tarafa ya Loliondo iliyopo wilayani humo pia alikagua ujenzi wa josho na upandaji wa nyasi kwa ajili ya kulishia mifugo.

"Serikali inataka kuwa na rekodi za mifugo yote na hili ni takwa la kibiashara na hii itasaidia serikali na ninyi wafugaji kwa kujua mifugo hii inatoka wilaya gani na nani anamiliki. Pia itasaidia kuimarisha masoko ya mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja kusaidia kudhibiti migogoro ya wakulima na wafugaji," alisema Ulega.

Kuhusu upandaji wa nyasi kwenye shamba lenye ukubwa wa hekari saba ambapo zitapandwa nyasi, alisema eneo hilo litakuwa la mfano wa wafugaji ili wapate majawabu ya ufugaji wa kisasa, huku wakitambua rasilimali mifugo ina utajiri mkubwa.

"Ni wakati muafaka sasa kwa wataalamu wa mifugo kuhakikisha wafugaji wa Wilaya ya Ngorongoro wanashirikishwa hasa katika shamba hili ili kila mmoja ajifunze na kupata uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa wa kupanda nyasi katika maeneo yao ili kukabiliana na ukame," aliagiza Ulega.

Katika hatua nyingine, Ulega aliwaagiza Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) kuweka huduma za maji sehemu za kunyweshea mifugo (mbauti) kulingana na aina ya mifugo wakati wa kutekeleza miradi ya maji, kipaumbele kiwe pia katika maeneo ya malisho kwani tayari Rais ameshatoa kiasi cha sh. bilioni sita kwa ajili ya ujenzi mbauti na visima nane vya maji.

"Mnapojenga mbauti hizi hakikisheni za ng'ombe kunywea maji ni tofauti na mbauti za mbuzi na kondoo ili mifugo yote iweze kunywa maji ya kutosha bila bughudha," alisema Ulega.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Uzalishaji wa Masoko, Fadhili Chamwazi, kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, alisema katika zoezi hilo la kuhimilisha mifugo ng'ombe 765 walikaguliwa, waliokidhi vigezo kuendelea na zoezi ni 575 huku 200 wakikosa sifa kutokana na kuwa na magonjwa ya uzazi na historia ya kutokupata mimba (ugumba).

Alisema wizara kwa kushirikiana na halmashauri imefanikiwa kujenga mradi ya majosho kwa ajili ya kuogesha mifugo ambapo kwa Wilaya ya Ngorongoro imepewa lita 400 kwa ajili ya kuogesha mifugo kwenye majosho 11 lengo likiwa ukinga mifugo na magonjwa ya homa ya mapafu.


## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA

**PONGEZI**

MWAKA 1 MADARAKANI



**Mhe.Samia Suluhu Hassan**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

#Samia 365

1. Kusajili dawa 724 ,vifa tiba 305 na vitendanishi 138 baada ya kujiridhisha na ubora, usalama na ufanisi wake
2. Kuendelea kushikilia cheti cha ithibati cha ISO 9001:2015 na ithibati kwa Maabara kiwango cha ISO/IEC 17025:2005
3. Kuongeza bajeti kulikowezesha utoaji huduma kwa ufanisi na kutoa gawio kwa Serikali kiasi cha Tsh bilioni 5.9
4. Kuendelea kutoa msaada wa kiufundi kwa viwanda vipya 15 vya dawa na 24 vya vifaa tiba nchini
5. Kuidhinishwa kwa Muundo wa TMDA na ongezeko la Watumishi kufikia 293
6. Matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika utoaji huduma za vibali ambapo sasa vinatolewa ndani ya saa 24
7. Kuendelea kushikilia ngazi ya Tatu ya WHO ya ubora wa mifumo ya udhibiti(Maturity Level 3)
8. Kusogeza huduma kwa wananchi kwa kujenga ofisi ya kanda ya kati
9. Kuanzishwa kwa Maabara za tumbaku na dawa za mitishamba mkoani Dodoma na Maabara ya vitendanishi jijini Dar es Salaam

"TMDA Hulinda Afya ya Jamii"


Scanned with CamScanner

# Mradi bandari ya uvuvi kuanza

**Elizabeth Edward**, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Serikali imesema ...di wa ujenzi wa bandari ya ...a unatarajiwa kuanza muda ...wote kuanzia sasa, baada ya ...kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

Bandari hiyo inayotarajiwa kujengwa Kilwa Masoko itaiwezesha sekta ya uvuvi kuchangia kikamilifu katika uchumi wa uvuvi.

**Mkurugenzi msaidizi wa utafiti na mafunzo ya uvuvi, Dk Erastus Mosha alisema hayo katika mkutano wa wadau uliolenga kupitia rasimu ya taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi huo wa kimkakati.**

Alisema bandari hiyo itaiwezesha nchi kupata mapato kupitia meli za uvuvi na bidhaa zinazotokana na uvuvi zitauzwa nchini.

Dk Mosha alisema Serikali imeona ipo haja ya kutenga fedha kufanikisha ujenzi huo unaotara... kufanyika katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa.

**03**

**Kiwango cha miaka ambacho mradi wa bandari ya uvuvi utatekelezwa**

"Tanzania hatujawahi kuwa na bandari ya uvuvi na hili limesababisha tumeshindwa kunufaika vya kutosha kupitia rasilimali za uvuvi, kwa ma... na meli kubwa zinazovua kw... nye ukanda wa uchumi wa baha... kushindwa kuja kwetu kut... mizigo yao," alisema Dk Mosha.

"Kutokana na mazingira hay... tumeishia kupata tozo ya le... ni ya hizo meli pekee, tukiac... mizigo yote wanayopata ... shughuli zote zinazohusu uv... na bandari zinaenda kufany... katika nchi nyingine tungeku... na bandari meli zingeweza k... kwetu."

Kaimu Mkurugenzi Idara ... Uvuvi, Merisia Mparazo alis... utekelezaji wa mradi huo u... wezesha nchi kuvuna rasili... zilizopo kwenye ukanda ... uchumi wa bahari, hasa kwa ... kina kirefu.

Scanned with CamScanner

# Tahadhari ugonjwa hatari katika nyama, maziwa

Kelvin Matandiko, Mwananchi
kmatandiko@tz.mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kimeonyesha wasiwasi wa ongezeko la ugonjwa wa 'kutupa mimba' unaoathiri mfumo wa uzazi kwa yeyote atakayekula nyama isiyoiva au maziwa yasiyochemka vizuri kutoka kwa ng'ombe aliyeambukizwa ugonjwa huo.

Ugonjwa huo unaojulikana kama Brucellosis, unasababishwa na vimelea vya bakteria wanaoshambulia kila aina ya mnyama hata binadamu endapo atakula au kugusa masalia ya wanyama wenye ugonjwa huo.

Mbuzi huambukizwa na bakteria aina ya Brucella melitensis. Ng'ombe (Brucella abortus), farasi (Brucella abortus au Brucella suis), nguruwe (Brucella suis), kondoo (Brucella ovis) na mbwa ni Brucella canis.

Mtalaamu wa afya ya mifugo na uzalishaji, Elias Uwiso alisema vimelea vya bakteria hao hubaki katika mfumo wa damu na kukaa katika maziwa na nyama ya ng'ombe aliyeambukizwa, hivyo binadamu anatakiwa kuchukua tahadhari kwa kuchemsha maziwa au nyama na kuhakikisha imeiva ili kuepuka maambukizi yake.

"Ukila nyama au maziwa ya ng'ombe huyo bila kuyachemsha vizuri utaambukizwa. Pia inaharibu mfumo wa uzazi kwa wanawake au wanaume," alisema Uwiso na kuongeza:

"Ni bakteria anayeishi kwenye nyuzi joto la kuanzia 20°C hadi 40°C inategemea na mazingira, pia anaweza kuishi kwenye mazingira kwa mwezi mmoja kama mnyama au masalia ya wanyama wenye ugonjwa huo hayakuhifadhiwa sehemu salama."



**NUKUU**

***"Ukila nyama au maziwa ya ng'ombe huyo bila kuyachemsha vizuri utaambukizwa. Pia inaharibu mfumo wa uzazi kwa wanamke au wanaume."***

**Elias Uwiso**

Katika mahojiano na gazeti hili hivi karibuni, Mwenyekiti wa chama hicho, Jeremiah Wambura aliwatuhumu maofisa wa maliasili na utalii kuendelea kukamata na kushikilia mifugo yao ndani ya maeneo ya hifadhi, hatua inayochochea ukuaji wa ugonjwa huo.

### *Kauli ya Serikali*

Mei mwaka jana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki kupitia hotuba yake bungeni alisema kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, likiwamo Shirika la FAO na WHO waliandaa na kuhuisha mikakati ya kuzuia magonjwa yanayoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama. Alisema mwaka 2020/2021 mitamba (ng'ombe wa kisasa) 162,843 ilichanjwa dhidi ya ugonjwa huo katika Wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma Jiji, Simanjiro, Iringa na Njombe. Katika kipindi hicho pia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ilitoa dozi 13,275 dhidi ya ugonjwa huo.

Kuhusu changamoto za kuenea kwa ugonjwa huo, alisema: "Tumezungumza nao (wafugaji) mara nyingi, tunawaambia wasiingize mifugo maeneo ya hifadhi kwa sababu ni rahisi kuambukizwa ugonjwa huo (wa kutupa mimba) lakini hawasikii, sijui kwa nini, hawaelewi."

Kuhusu madai ya kushikiliwa ng'ombe eneo la hifadhi, Ndaki alikiri ni kweli sheria hairuhusu, lakini baadhi ya wafugaji wamekuwa wagumu kuzingatia maelekezo ya Serikali. "Lakini si ng'ombe wote wanaoambukizwa wanakamatwa, kuna wafugaji wanachunga wenyewe maeneo ya wanyama, tutaendelea kusimamia sheria," alisema.

Scanned with CamScanner